


# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | Aug-2022

EAJK

# Uhalisia katika mashairi ya Kezilahabi (Dhifa)

**Author**
**Jane Kanini Maithya**
**Email:** maithyajk@gmail.com

**Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Maithya, J. K. (2022). Uhalisia katika mashairi ya Kezilahabi (Dhifa). *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 1(1), 43-49. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.183

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 10.07.2022
Accepted: 15.07.2022
Published: 15.08.2022

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2022 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY) and their terms and conditions.

**Ikisiri**
Fasihi ni kioo cha maisha. Humulika jinsi jamii ilivyo kwa kuangazia masuala mbalimbali yanayoikumba. Waandishi wa kazi za fasihi huchota maudhui yao kutokana na matukio mbalimbali yanayoikumba jamii, nia yao ikiwa ni kuielimisha, kuiadilisha na kubeza maovu yanayotendeka. Makala hii inaangazia uhalisia katika mashairi ya Diwani ya Dhifa iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi (2008). Kupitia kwa mashairi yake, Kezilahabi ameichora hali halisi iliyopo katika mataifa mengi ya Afrika kwa kumulika matatizo mbalimbali yanayoyakumba. Anaupitisha ujumbe wake kwa kutoa taswira nzito zinazoundwa kutokana na matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi ambazo zinaacha athari kubwa kwa wasomaji na kuwachochea kupata ari ya kupigania haki za wanyoge. Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya uhalisia, ambayo kulingana na Wamitila 2002, iliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake kinachojulikana kama Aesthetik. Utafiti unawawezesha wanajamii hasa kutoka mataifa ya Kiafrika kuyabaini matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo na jinsi ya kujinasua kutokana na minyororo ya umaskini.

**Maneno muhimu:** Uhalisia, tashihisi, tamathali za usemi.

**UTANGULIZI**

Diwani ya Dhifa iliandikwa na Euphrase Kezilahabi (2008). Ni diwani iliyo na mashairi sitini ambayo yote ni huru. Kezilahabi ni mwandishi mtajika sio tu katika nyanja ya ushairi bali pia katika utanzu wa riwaya. Katika diwani ya Dhifa, mshairi anataka wasomaji wake wadadisi, wahoji, wachunguze na kuzichokonoa nafsi zao, mazingira yao, siasa yao, nchi yao, ujitambuzinafsi wao na hata maisha yao yenyewe (Kezilahabi 2008). Mshairi anayazungumzia masuala mengi yakiwepo utawala mbaya, ukoloni mamboleo, umaskini na kifo. Hii ni diwani iliyokitwa kwenye kupiga darubini falsafa nzima ya maisha ya binadamu katika duara yake ya maisha yanayoanzia kwenye mji wa mamake na kuishia kwenye mji wa kaburi.

**Mtazamo wa Uhalisia**

Mtazamo wa uhalisia humulika hali halisi ya jamii bila kupunguza wala kuongeza chochote. Ni mtazamo ambao Wafula na Njogu (2007) wanadai kuwa muhimu zaidi kutokea katika karne ya kumi na tisa na ishirini na pengine utaendelea kutuathiri katika karne ya ishirini na moja. Wamitila (2002) anasema kuwa dhana ya uhalisia hutumiwa kwa maana mbili kuu. Kwanza, kuelezea tapo la kipindi maalum cha kihistoria katika fasihi za Ulaya. Pili, kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambapo kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Kulingana naye, kazi ambazo huangaliwa kama za kihalisia zinatarajiwa kumulika hali halisi ya maisha katika jamii husika. Anasema kuwa neno uhalisia huelezea kazi za kifasihi ambazo huwakilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda jambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali iliyomo.

Kulingana na Wafula & Njogu (2007), uhalisia wa kifasihi huashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana binadamu. Mwandishi anayeongozwa na nadharia hii hujibidiisha kuonyesha ukweli jinsi ulivyo na kuonyesha picha kamili ya mazingira ambamo mwanadamu anajipata. Wanasema kuwa mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. huweza kusuta maovu katika jamii kwa kuwatetea watu fulani na kuwasuta wengine kulingana na msimamo wake.

Wafula (1992) anasema uhalisia ulitokea kwa sababu za kihistoria. Wachache wenye kumiliki njia za kuzalisha mali walijibidiisha kujiimarisha huku wakitumia nguvu za wanyonge. Wanyonge walichoka na dhuluma kisha wakaungana kudai haki zao. Msokile (1993) anasema kuwa nadharia hiyo ilianza kupata nguvu wakati wa Eliot George wa Uingereza na kufikia leo kuna aina nyingi za uhalisia kama vile uhalisia wa kibwanyenye, uhalisia wa kijamaa na uhalisia wa kiyakinifu. Kulingana naye, mwanahalisia anastahili kushughulikia mambo yote bila kupuuza jambo lolote katika jamii.

Momanyi (1991) ana maoni kuwa ikiwa fasihi itaweza kuchukua jukumu la kusuluhisha matatizo yaletwayo na mielekeo mipya katika jamii, jukumu ambalo limesababishwa na historia, lazima kuwe na waandishi wa kifalsafa na kisiasa ambao ndio huzaa fasihi. Kezilahabi katika kuupitisha ujumbe wake kwa wanajamii amezungumzia maudhui mbalimbali ambayo yanatoa picha kamili ya matatizo mbalimbali yanayowakumba watu katika mataifa mataifa ya Afrika. Baadhi ya maudhui ni:

**Ukoloni Mamboleo**

Shairi la *Dhifa* limetungwa kumulika uongozi katika Bara la Afrika. Kezilahabi anazungumzia wakati wa ukoloni ambapo Wazungu na Waarabu Waling'ang'ania na kuligawa Bara la Afrika kwa manufaa yao wenyewe (Mbaabu, 1996). *Dhifa* ni jazanda ya mkoloni kusherehekea baada ya kufaulu kuzinyakua na kuzitawala nchi mbalimbali za Afrika. *Bwana Mkubwa* katika shairi hilo ni taashira ya viongozi wanaotawala kwa unafiki na *kamasi* ni taswira inayoashiria uovu. Uovu unaozungumziwa ni dhuluma dhidi ya watawaliwa, uonevu, ubaguzi wa rangi, unyonyaji na unyang'anyi wa raslimali za umma. Kimsingi, mfumo wa uongozi ulihakikisha kwamba mataifa ya kikoloni yananufaika kwa vyovyote vile. Mtunzi anasema, *"Nzi atua pale na kulila kamasi."* Anaashiria hali ya viongozi kufurahia matunda ya uongo wao na kushabikia unafiki. Kezilahabi anabainisha kuwa wanaonufaika kutokana na mfumo huo ni mawaziri ambao hupata pesa nyingi, wabunge

wanaopewa magari na waandishi wa habari, huku maskini wakibaki nyuma bila kupata chochote.

Katika shairi la *Njia Tulopitishwa*, mtunzi anaashiria athari za mfumo wa kikoloni wa ubepari. Anaeleza kwamba mfumo wa kibepari umekita mizizi katika jamii ya sasa. Anasema "Sasa wakokota tongotongo nzito machoni kwa mswaki kuukuu." Mswaki kuukuu ni ishara ya mbinu ambazo zinatumika kuondoa athari za mfumo wa kikoloni na ambazo hazina nguvu tena ya kukabiliana na uozo uliopo katika jamii. Hata wale wanaotegemewa kuleta mabadiliko ni zao la mfumo huo. Kezilahabi anasema, "Kisha wanacheka gizani kwa mawi yatokeayo." Anamaanisha kuwa wanaendesha mambo yao gizani kama vile ulaghai na wanafurahia tendo hilo. Hata hivyo, ana matumaini kuwa siku moja haki itatendeka.

**Tamaa.**
Nchi nyingi za Afrika zimeangamizwa na tamaa ya viongozi. Rasilmali za nchi badala za kuwafaidi wananchi zinawafaidi viongozi wachache. Shairi la *Madomo Mapana* linaonyesha hali ya kusikitisha ya wanyonge kutokana na kuwepo kwa viongozi ambao wanajifikiria wao wenyewe bila kujali maslahi ya raia na nchi wanazotawala. Raia wanateseka kutokana na mfumo wa kibepari ambapo viongozi hudhibiti njia zote za uzalishaji mali. Watawaliwa hunyonywa jasho lao, hawafurahii matunda ya jasho lao wala uhuru walioupata. Mtunzi anatumia tashbihi kuwachora wanasiasa kama wezi wanaoiba mali ya umma bila kujali kizazi cha kesho.

Katika shairi la *Jibwa,* mtunzi anaonyesha kuwa viongozi wenye tamaa wakiwa uongozini tamaa yao huongezeka na hawatosheki wala kujali utu na maslahi ya wengine. Anaeleza kuwa jibwa likianza kuiba huwa na mazoea ya kuendelea kuiba na huanza na mayai (vitu vidogovidogo). Kezilahabi anasema, "Kesho litakula kitovu cha mtoto wako pekee, jibwa jizi fisi." Kula kitovu cha mtoto ni sawa na kula kiini cha maisha yake. Hii ina maana kuwa viongozi kama hawa wanaweza kuangamiza chemichemi za maisha ya walio wengi.

Shairi la *Cha Watu* limetumiwa kuwakashifu wazee waliopigania uhuru ambao wana tamaa ya mali. Mtunzi anasema, "Udenda wao umedondokea chakula." Anamaanisha kuwa kwa sababu ya tamaa yao ya kupita kiasi, wamekula raslimali yote ya taifa. Wameifilisi nchi na sasa wanajaribu hata mifupa. Mtunzi anaashiria kuwa nchi nyingi za Afrika ziko hatarini ya kuanguka kiuchumi kutokana na tamaa ya viongozi.

Shairi la *Jibwa* limetumiwa kubeza tamaa ya viongozi vilevile Mtunzi anasema:

Jibwa likishika hatamu
Haliwezi kuacha tamu
Litatumia kila hila
Litakacho likipate

Kezilahabi anasema kuwa dawa ya jibwa hilo ni shoka. Anasema kuwa viongozi wenye tamaa hawawezi kung'oka uongozini ila waangamizwe au wang'olewe uongozini kwa nguvu.

**Utabaka**
Katika shairi la *Dhifa*, Kezilahabi anabainisha kuwa wanaonufaika kutokana na mfumo wa ubepari ni mawaziri ambao hupata pesa nyingi, wabunge wanaopewa magari na waandishi waliopewa kazi. Wazungu, Wahindi na Waarabu wanaitwa walanchi kwa sababu pia hunufaika kutokana na mfumo wa kidhalimu unaotawala nchi nyingi za Afrika. Mazingira yanayoibua shairi hili ni mfumo wa utabaka usiojali maslahi ya walio wengi. Katika shairi la *Maendeleo si Ndwele*, mfumo wa kibepari unaoendelezwa ili kuwakandamiza wanyonge katika jamii unamulikwa. Tabaka tawala lilitumia mbinu na hila mbalimbali kulinda na kudumisha maslahi yao kiuchumi. Azimio lililenga kuleta usawa wa kiuchumi, kuondoa utabaka na ubinafsi. Hata baada ya kutangazwa kwa Azimio, kulikuwa na pingamizi kutoka kwa wale walioendeleza mfumo wa ubepari. Mshairi anasema 'Watoto wanagongana wao kwa wao'. Hapa anamaanisha kuwa hata wale waliokuwa na mawazo mazuri baada ya uhuru na azimio wameathiriwa na mfumo wa kikoloni wa kupigania kipato.

Katika shairi la *Ukweli Koko*, mwandishi ametumia kinaya anaposema, *"Watawala wa Afrika ni wapenda demokrasia, umaskini ni wa kujitakia."* Ukweli ni kuwa watawala hao wanakiuka demokrasia ili kujilimbikizia mali huku wananchi wakizama kwenye lindi la umaskini. Shairi hilo linaonyesha jinsi utawala uliopo umejaa unyonyaji na ukandamizaji. Ni uongo kuwa

umaskini ni wa kujitakia na wafanyakazi ni wavivu. Mfumo wa udhalilishaji ndio unaowaumiza na kuwafanya walimao wasivune mazao ya jasho lao. Kwa kusema kuwa ardhi, madini na nafaka ni mali ya umma ni uongo kwa sababu ni mali ya walio wachache au mali ya umma lakini kwa manufaa ya walio wachache.

Shairi la *Maskini* linamulika udhalimu wa kitabaka ambapo tabaka la juu linalidhulumu tabaka la chini. Maskini wanaendelea kukandamizwa hadi kufa kutokana na mfumo dhalimu usiojali watu wanaoishi katika ulitima. Kazilahabi anasema, "*Maskini amechinja maelfu ya sisimizi, chajio cha mwisho.*" Maskini kutokana na kukosa chakula wanakula wadudu na tunaambiwa ndicho chakula chao cha mwisho kabla hawajakufa kutokana na njaa. Ni kinaya kuwa maskini akifa, wanajamii wanamtupia majani wasipatwe na laana ilhali walikuwa katika nafasi ya kumwokoa lakini hawakumpa chakula.

**Ukengeushi**

Kukengeuka ni kudunisha mila na tamaduni za jamii ya mtu na kufuata mila na tamaduni za jamii geni. Kezilahabi anasema kuwa kukengeuka kwa Waafrika kumechangia kuzorota kwa maendeleo hasa katika nchi za Afrika. Shairi la *Ukweli Koko* limetumiwa kuonyesha ya kwamba Kiingereza na Kifaransa ni funguo za maisha. Hali hii inatokana na sababu kwamba Waafrika hupuuza lugha zao za kienyeji na kutukuza za kigeni wanazozihusisha na ustaarabu. Kazelahabi ana maoni kuwa elimu ya kikoloni hutumikia uchumi wa kibepari. Hali hii imemfanya Mwafrika kuwa mtumwa katika mazingira yake. Kuwa lugha za Afrika ni lugha za mtaani ni kuonyesha jinsi tumezidharau lugha zetu za asili. Hii ni njia ya kuendeleza ukoloni mamboleo.

Shairi la *Mke wa Waziri* linaonyesha jinsi binadamu hujisahau hasa anapotoka katika tabaka la chini na kuanza kuona walioshiriki naye kama watu duni. Monika alibadilika alipofika mjini na kuolewa na waziri. Tukio hili linamwathiri Monika kitabia, kimtazamo na kimwenendo. Kezilahabi anasema:

*Upitapo wainua kipua juu*
*chogo limechongoka kama senene*
*Aendaye kwenye harusi ya mende*

Mtunzi anamsifu mwanamke anayeishi mashambani ambaye licha ya kudunishwa na kuonekana mshamba, hufanya kazi muhimu ya kulima na kupalilia mimea ingawa wanaonufaika kutokana na jasho lake ni matajiri.

**Nafasi ya Vijana**

Shairi la *Marahaba* linaonyesha haja ya watu kujitambua na kujua kuwa yafaa waishi maisha adilifu na kutumia nguvu zao kwa busara wakiwa vijana. Anaonyesha kwamba watu wanavyozeeka ndivyo matatatizo yao ya maisha yanavyoendelea kuongezeka. Hii ina maana kwamba ni muhimu watu kupanga maisha yao ya baadaye kama wangali wana nguvu. Shairi hili linaonyesha kwamba vijana wana nafasi muhimu katika jamii. Wana nguvu na wanaweza kutekeleza mambo mengi.

*Wimbo wa Unyago* ni shairi linalowasisitizia vijana kuishi maisha yao na wazee waishi yao. Ili vijana waweze kuishi vizuri, wafaa kuepukana na ukabila. Anawashauri wasichana waolewe kulingana na mapenzi yao bali si kushurutishwa. Shairi la *Cha Watu* linakashifu wazee waliopigania ukombozi kuchukulia nchi kuwa ni yao. Wazee hao wamekatalia uongozini huku vijana wakiambiwa wao ni viongozi wa kesho. Wazee hao huwaona vijana kama watu wasio na tajriba ya kuongoza.

**Haki za Wafanyakazi**

Shairi la *Kwa Walimu Wote* limetumiwa kuonyesha dhiki zinazowakumba wafanyakazi wa serikali kama vile walimu. Anachora taswira ya shida wanazopitia walimu wakistaafu kama vile viatu vilivyoisha visigino, sidiria chakavu na chupa tupu za pombe na marashi. Umaskini huu unatokana na mshahara duni wanaolipwa hivi kwamba hawawezi kujiwekea akiba ya baadaye. Umaskini unamfanya mwalimu kudharauliwa. Mtunzi anasema, "*Nilipokuwa mwalimu nikaitwa bure.*" Hata hivyo, Kezilahabi anainua hadhi ya mwalimu kwa kusema wana ushawishi mkubwa kwa hivyo wanastahili kuwafunza watu kushirikiana na kuachana na unafiki.

Shairi la *Ukweli Koko* linaonyesha jinsi jasho la wakulima linawafaidi wengine. Wakulima wana mateso mengi kwa sababu ya kunyanyaswa na mfumo uliopo. Mfumo wa kibepari wenye ukiritimba

unawanyonya wafanyakazi na kuwasingizia kuwa wavivu. Mshairi ametumia kinaya kubeza viongozi wa Afrika ambao ni wenye tamaa na ndio hunufaika kutokana na jasho la wakulima huku wakidai ardhi na fanaka ni mali ya umma. Shairi la *Alalaye* ni mfano wa dhiki zinazowakumba wakulima na wavuvi. Mtunzi anasema kuwa huku wakulima na wavuvi wakiendelea kuumia, wale wanaofaa kuwaokoa hawajali. Mtunzi anaposema *mafuriko yaliyotokea* anaashiria hali inayoathiri masoko ya ulimwengu ambayo hutangaza bei ya chini, jambo ambalo huwapunja wakulima na wavuvi. Mtunzi anaendelea kusema, "*Tumeona mifupa ya kuku jalalani.*" Kauli hii inaashiria kwamba wakulima na wafugaji wameshuhudia ishara kwamba kumekuwepo na manufaa yanayotokana na jasho lao lakini hawakushirikishwa katika uhondo huo. Hii ina maana ya kwamba jasho lao linawafaidi wengine.

**Ndoa**

Katika shairi la *Msamaha,* Kezilahabi anaonyesha umuhimu wa msamaha katika maendeleo ya jamii hasa familia. Anaeleza kuhusu mhusika ambaye ametambua makosa yake na sasa anaomba msamaha. Kulingana na mtunzi, mhusika alimdhuru mkewe na kumsababishia madhara makubwa Taswira ya uso kuvimba inaashiria kwamba mume alimpiga mkewe. Mume anakiri ya kwamba hakushawishiwa na pombe wala hasira bali ni yeye mwenyewe. Hatua hii inaonyesha uponyaji unaweza kupatikana katika ndoa na jamii iwapo wanaohusika watatambua makosa yao.

Katika shairi la *Wimbo wa Unyango*, mtunzi anashauri wasichana waolewe kulingana na mapenzi yao bali si kushurutishwa. Kezilahabi anawaambia vijana waoe au kuolewa na wanaowataka bila kuzingatia ukabila. Aidha, wasikubali kusikiliza umbea wa wanaowaambia waume zao ni wabaya. Anasema kuwa ili jamii ipate kuendelea, kuna umuhimu wa kupanga uzazi. Wito ni kwamba watu wazae idadi ya watoto ambao wataweza kuwalea huku wakitunza afya zao kwa kuepuka kuzaa watoto wengi.

**Mapinduzi na Ukombozi**

Kezilahabi amezungumzia sana maudhui ya mapinduzi na ukombozi. Katika shairi la *Walimu Wote,* mtunzi anamhamasisha mwalimu kuwazindua wanafunzi wake kuhusu haki zao badala ya kutunga nyimbo za kuwasifu viongozi dhalimu. Vilevile, anawahamasisha wananchi wote kwa jumla kuwa ikiwa wangetaka mabadiliko, lazima waungane pamoja na kupiga kura ili kuwaondoa viongozi dhalimu mamlakani. Mtunzi anawaona walimu wana nafasi muhimu kwa vile wana busara na wanaweza kuuzindua umma kupitia kwa kuielimisha jamii.

Shairi la *Madomo Mapana* linaashiria kifo cha wanasiasa dhalimu kitatoa suluhu kwa walio wengi kupata afueni. Wananchi pia watajikomboa kutokana na mfumo dhalimu. Mtunzi anasema:

> Mwanasiasa afapo
> Tumejikomboa na domo
> Moja pana lizibwalo na mchanga

Katika shairi la *Jibwa*, mtunzi anasema ni muhimu kupambana na viongozi wanaoendeleza hulka za kikoloni ili kuwaangamiza kabisa. Hii ndio sababu anasisitiza wito wa *kulipiga jibwa kichwa, kulimwagia petroli, kulifunga kamba shingoni na kuliburuzwa hadi jalalani.* Anasema ya kwamba huwezi kupigana nao ana kwa ana. Ni muhimu kuwapangia mikakati ya kuwaangamiza kisiasa kwa kupiga kura kwa busara ili kuwaondoa uongozini. Katika shairi la *Mafuriko,* mtunzi anawahamasisha wananchi kuhusu uchaguzi bora wa viongozi. Anabainisha ya kwamba ni kutokana na uchaguzi bora tu ambapo viongozi wa zamani wataweza kuondolewa madarakani. Mafuriko anayoyazungumzia mtunzi ni mapinguzi kupitia kwa upigaji kura kwa busara ili kubadilidha viongozi wanaoendeleza uongozi mbaya, jambo ambalo litasababisha ujenzi wa jamii mpya hasa katika nchi za Afrika. Wananchi watawachagua tu viongozi wenye maono.

**Uongozi Mbaya**

Maudhui ya uongozi mbaya ambalo ndilo tatizo kuu katika nchi nyingi za Afrika yamejadiliwa kwa kina kupitia kwa mashairi mengi katika diwani ya *Dhifa*. Shairi la *Ulingoni* linazungumzia mfumo wa uongozi ambao haukubadilika hata baada ya uhuru. Licha ya miaka mingi ya uhuru, hakuna chochote ambacho kilionyesha matunda ya uhuru. Hata baada ya miaka mingi ya uhuru, ukoloni mamboleo na ubepari ni vitu ambavyo vilihitaji kushughulikiwa kwa kutumia mbinu na mikakati mipya. Mtunzi anaonekana kutumia lugha

kali ya matusi ili kuwabeza viongozi dhalimu anaposema, "*Wanacheza matako nje wala hawapendezi. Na hakuna awashangiliaye.* Wananchi hawafurahii nyimbo zinazochezwa ulingoni kutokana na dhuluma wanazofanyiwa na viongozi.

Shairi la *Maendeleo si Ndwele* linaonyesha jinsi uongozi mbaya umesababisha umaskini katika Bara la Afrika. Mtunzi anasema, "*Baba atoka chumbani na bunduki akiyumba*. Hii inamaanisha kwa kukosa mwelekeo, kiongozi wa taifa anatoka na kauli kali ya kuangamiza maovu, lakini pia anayumbayumba kwa kukosa msimamo thabiti. Inaamaanisha pia yeye ameathirika. Kezilahabi anasema, "*Akiimba wimbo wa Taifa wa Afrika." Anaashiria* kuwa wao ni wamoja katika taifa moja la Afrika.Wimbo huu ni ishara ya unafiki kwa kuwadanganya watawaliwa kwamba wako pamoja ilhali mipaka ya utabaka inandelea kupanuka. Mshairi anasema, "*Wimbo aliotunga akiwa ndotoni."* Hapa anaashiria mambo mazuri anayowaza tu lakini hatendi. Uongozi mbaya umesababisha umaskini katika mataifa ya Afrika.

Shairi la *Madomo Mapana* linaangazia ulafi wa viongozi ambao unafananishwa na zimwi ambalo husukuma mtoto pembeni ili linyonye maziwa ya mama yake. Kifo cha viongozi hao ni furaha kwa wananchi kwa vile hawana umuhimu ila kuifilisi nchi. Mtunzi anawaona walimu ndio wenye busara na ndio wanapaswa kuiongoza nchi kwa sababu hao ndio huona mbali. Anasema:

> Nchi mmeifilisi waachieni walimu
> Wakajenge taifa jipya
> Kama hamwezi kuona mbele

Katika shairi la *Dhifa,* Kezilahabi anawaita Wazungu, Wahindi na Waarabu walanchi kutokana na tabia yao ya kulipora Bara la Afrika. Mawaziri na Wabunge wanakula na kuishi maisha ya kifahari huku maskini wakiteseka. Viongozi hao wanalinganishwa na nzi wanaokunya kutokana na shibe huku maskini wakiangamizwa na njaa. Mtunzi anawafananisha viongozi hao na zimwi ambalo limemeza watoto wote kijijini katika shairi la *Zimwi.* Taswira hiyo imetumiwa kuonyesha jinsi viongozi fisadi huangamiza maisha ya kesho ya watoto wetu kutokana na tamaa na ufisadi. Wanakijiji wanalifuata wakitaka kuliangamiza huku wakiongopa hatari iliyopo kwa vile zimwi lina nguvu. Viongozi hao wanaogopwa na wananchi kwa sababu wamelindwa na vyombo vya dola. Ni mazimwi ambayo ingawa yanatujua yanatula na kutumaliza.

**Dhuluma**

Katika shairi la *Makaburini*, Kezilahabi anaeleza masaibu yanayowakumba watoto yatima. Msichana husingiziwa umalaya na mvulana kuambiwa ya kwamba ameambaa tabia ya ulevi kama babake. Ni bayana kwamba mayatima wanateseka sana mikononi mwa jamaa zao wanaofaa kuwalinda. Watoto hao wanateseka kwa kufanywa wafanyakazi wa kazi duni kama vile kuuza kwa baa badala ya kupelekwa shuleni wapate elimu. Shairi la *Hoja* linadhihirisha kuwa unyanyasaji umekithiri katika jamii. Watu hawajali hisia za wenzao. Mtunzi anatuchorea taswira ya namna wanyonge wanavyoangamizwa. Ni kinaya kwamba maovu kama vile ubakaji, unyanyasaji na uonevu hasa kwa wanyonge yanaendelea na hakuna anayejali.

**Nafasi ya Mwanamke**

Katika shairi la *Binti,* mtunzi amemchora mwanamke kama kiumbe duni ambaye kazi yake ni kuwafurahisha wanaume. Anamsihi akatae kuwa *ubao wa matangazo* au *vilabu vya mpira.* anamhamasisha mwanamke ajihisi huru na atende yanayomridhisha. Anamshauri kupigania haki zake katika jamii inayomsawiri kama kiumbe duni na apate elimu itakayomsaidia kujinasua kutokana na minyororo ya utumwa. Mtunzi katika Shairi la *Hoja* anabeza ubabedume unaoendelezwa na jamii dhidi ya mwanamke. Analinganisha kisa alichokisoma cha kijana akimbaka msichana wa miaka kumi na sita na simba anayemfukuza pundamilia. Anasema dhuluma ya ubabe inaweza kuharibu umma.

**Umaskini**

Kezilahabi amezungumzia maudhui ya umaskini kwa kina katika shairi la maskini. Maskini hupuuzwa na kuonekana kuwa watu wasio muhimu. Katika shairi hili, maskini anasema kuwa ananongwa na njaa na amekondeana kama siafu. Hakuna anayesikia kilio chake cha mateso. Matajiri wameweka nta kwenye masikio yao ili wasisikie kilio cha wanyonge. Licha ya kuwa nchi yenyewe ni tajiri, wanaonufaika ni matajiri huku maskini wakila makombo yaliyobaki.

> Nikinywa maji ya mvua
> Yaliobaki juu ya jani la mti

Wa utajiri utiririkao kama mto.

Shairi la *Kwa Walimu Wote* linaonyesha kuwa licha ya walimu kutoa mchango mkubwa katika jamii, wanapostaafu huishi maisha ya uchochole.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu
Mijusi watatega mayai ndani ya viatu
Vyako vilivyoisha visigino
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu
Za marashi na bia

Hali hiyo inatokana na mshahara duni wanaolipwa walimu ambao hauwezi kuwawezesha kuweka akiba ili wawe na maisha mazuri ya baadaye.

Katika shairi la *Maskini 11,* mtunzi anasema maskini anakula chakula chake cha mwisho ambacho ni sisimizi. Kula sisimizi kunatokana na kukosa chakula bora cha kula kutokana na umaskini. Anapokufa kwa njaa, hakuna anayeathiriwana na kifo chake. Wapita njia hawajali wanamwona alikufa kutokana na laana ya kuwa maskini.

**Kifo**

Katika shairi la *Wazo Nje ya Wakati,* mtunzi anatumia mbinu ya tashihisi kuonyesha kuwa kifo hakina huruma. Anasema kuwa kifo hufurahia watu wanapopatwa na magonjwa kama kansa, magari yanapogongana, ndege zinapoanguka na kunapotokea vita. Mtunzi anakiita kifo wazo nje ya wakati, kumaanisha ni kitu kisichoeleweka na kutabirika. Anatufahamisha kuwa lazima kila mwanadamu atakufa kwa hivyo hamna haja ya kuogopa kifo. Shairi la *Makaburini* linamulika matatizo wanayoyapitia watoto mayatima baada ya vifo vya wazazi wao. Watoto hao huonekana kuwa mzigo na walezi wao. Chochote kinachopotea huambiwa wao ndio wameimba. Wavulana huitwa wezi kama baba zao na wasichana malaya kama mama zao. Hunyimwa elimu huku jamaa za wazazi wao waking'ang'ania ardhi ya wazazi wao. Kazi yao huwa ni kuwauzia wateja bar iliyokuwa ya wazazi wao. Katika shairi la *Mahojiano na Kifo,* Kezilahabi anajibizana na kifo akikiambia hakina hisia. Anasema kuwa kifo hakibagui matajiri wala maskini, vijana na wazee. Kifo hakina jibu lolote kwa sababu shutuma zote zinazoelekezwa kwake ni za kweli. Shairi la *Marahaba* linaeleza hali ya watu kujitambua na kujua kuwa yafaa waishi maisha adilifu. Mtunzi anatuhimiza kuelewa hapa duniani sisi ni wasafiri. Maisha yetu ni mafupi kwa hivyo tujue namna ya kuishi. Tukiishi vyema, hatima yetu pia itakuwa njema. Mtunzi anaonyesha kuwa maisha ya sasa yana changamoto nyingi. Changamoto hizi zimechangiwa na usasa ambao umewafanya wanajamii kugongana. Kwa mujibu wa mtunzi miongoni mwa mambo yanayotokana na usasa ni utovu wa maadili.

**MAHITIMISHO**

Makala hii inamulika maudhui mbalimbali anayoyaeleza Kezilahabi katika diwani yake ya *Dhifa.* Anazungumzia masuala mbalimbali yanayoiathiri jamii katika mataifa mengi ya Afrika. Baadhi yao ni umaskini, uongozi mbaya, dhuluma, matatizo anayozikumba ndoa na mengineyo. Nia yake ni kuwachochea wanajamii watafakari kuhusu hali inayowakumba na wapate ari ya kujinasua kutoka kwenye minyororo ya maonevu.

**MAREJELEO**

Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide-Muwa Daisy Publishers Limited.
Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Afrika: A Dependency Theory Perspective.* Educational Research and Publications.
Momanyi, C. (1991). *Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-inkishafi*. Unpublihed M.A Thesis, Kenyatta University.
Msokile M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.
Wafula R. M. & Njogu K. (2007). *Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
Wafula, R. M. (1992). *Nadharia kama Mwongozo wa Utunzi na Uhakiki,* Makala ya Semina, Chuo Kikuu cha Nairobi.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.